

## **Kiangazi Kimefika!**

Nakumbuka jarida au hotuba ambayo mtu alihubiri miaka mingi iliyopita, kichwa cha hotuba hiyo kilikuwa “Kiangazi kimefika, na nguo zadondoka.” Ama kweli ni bahati mbaya kwamba jambo hili ni kweli. Mnamo 1999, Becky na mimi tulirudi Marekani kwa ajili ya Becky kujifungua mtoto William. Ilikuwa ni muda mrefu tangu tulipoondoka Marekani. Sitakuja nisahau jambo moja lililonitokea. Mavazi! Au ukosefu wa mavazi. Si kwamba sikuwahi kuona uvaaji usio wa staha, Bali tulikuwa tuko nje ya Marekani kwa miaka mitatu hivi, bila kuona uvaaji usio wa staha; na tulipoona, ilikuwa hivi; “unaweza kuamini kuwa wamevaa vile?” Ilikuwa ni nyakati karibu hizo hizo ambapo kwa Tanzania mwanamke akivaa jinsi angepigwa kwa mawe. Au kama wangemwona msichana akiwa amevalia suruali hata isiyobana walikuwa wanamshuku mabaya. Kwa hiyo wanaume bado wanavaa suruali na mashati. Ni mara chache kumwona mwanaume amevaa kaptula. Hata hivyo, huko ni Ikweta ambako ni joto na kukame kweli kweli. Na muda wote mwanamke anavaa blauzi na Khanga ndefu inayofunika hadi visigino. Kisha fikiria kuishi kule kwa miaka na sehemu kubwa ya ngozi unayoweza kuona kwa mwanamke ni shingo, uso, mikono, visigino na miguu. Kusafiri masaa 24 na kushuka Dallas mwezi wa tisa. Hee! Becky hivi uliona?

Hivi kuwa na vivazi vya nusu uchi Marekani leo, ni kwa sababu tumezoea kuona hii dhambi? Kwamba hatuoni aibu tena na haitusumbui, na hivyo tumeikubali hali hii kama hurka yetu na kufanya hivyo hivyo? Walakini hata kama hicho ndicho kisa; Na jamii inakubali mtindo fulani au aina fulani ya uvaaji. Hata kama tunaona kama kila wanachovaa watu leo kinakubalika, hayo yote, bado haibadili anavyofikiri Mungu! Namaanisha kwamba watu wengine huamini kuwa Mungu hayupo. Na bado haibadili ukweli kuwa Mungu yupo na anachofikiria. Lakini kwa habari ya mavazi ya staha, kama ilivyo katika mengine, Mungu hajatuacha pasipo ushuhuda

Kwanza, katika Mwanzo 3, baaada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi. Wakatambua wako uchi, na wakajifanyia mavazi fulani. Inawezekana mavazi yale hayakusitiri chochote zaidi ya kuwa kama vinguo vya kuogelea vya siku hizi. Lakini waliridhika kuvaa nguo zile kwa kuwa walikuwa mume na mke, hapo sawa. Walikuwa mume na mke. Lakini alipokuja mtu mwingine katika taswira hiyo, walikimbia. Kwa sababu kilichoonekana sawa walipokuwa wawili, alipokuja mwingine hakikuwa sawa tena. Ndipo Mungu akaamua kuwatembelea, nao wakajificha. Naye Mungu akawauliza, “kwa nini mmejificha?” nao wakajibu, “tuko uchi” Halafu katika 3:21 twasoma ya kwamba Mungu akawashonea nguo “akawavika”. Aliwafundisha tangu mwanzo uvaaji wa staha anaotaka..

Pili, Katika Kutoka 28, Mungu alikuwa akimwelekeza Musa kuhusiana na mavazi ya makuhani. Na katika Kutoka 28:42, Mungu akamwambia Musa, ‘ Nawe wafanyie suruali za nguo za kitani, ili kufunika tupu ya miili yao; suruali hizo zitafika tangu kiunoni hadi mapajani” Sasa, hii ilikuwa kwa mwanaume. Ni wazi kwamba hapa Mungu hazungumzii wanawake. Lakini haihitaji maelezo, kwamba endapo Mungu anaona ni utupu kwa mwanaume kuonyesha mapaja, ndivyo itakavyokuwa kwa mwanamke.

Tatu, katika Isaya 47, Isaya alikuwa anatabiri juu ya anguko la Babeli. Na kujaribu kukimbia kupitia mto anaeleza kuwa ni bikira (mistari 2-3). Mungu anaeleza kuwa utupu wake

utaonekana. Kwa nini? 1) Utaji wake ungeondolewa, 2)Kanzu yake ingeondolewa, 3) Miguu yake ingeachwa utupu. Matokeo yake ni kwamba miguu isiyofunikwa, mbele za Mungu ni utupu.

Kuna mwongozo dhahiri katika Biblia kwamba vazi lolote linaloonyesha ngozi iliyo juu ya mapaja huchukuliwa kuwa utupu. Kwa hiyo, ni kiangazi. Joto litaanza. Watu wataanza kusema, kuna joto kali, tuvue nguo. Kweli? Au huo ni udhuru wa kuvaa unachotaka kuvaa? Nimeishi katika nchi ambayo ni ya joto kali na kame kuliko hii. Nchi ambayo wanaume wote bado wanavaa suruali na mashati. Na wanawake bado wanajifunika kama Mungu anavyotaka, na hawayeyuki.

Kiangazi hiki, tusiache vipeperushi vya orodha, tovuti, au jamii iseme ni halali kuvaa. Tumuulize Mungu analofikiria. Na majibu tuyapate kwenye neno lake.